## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA TATU

**08 SEPTEMBA, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 08 SEPTEMBA, 2016

**I. DUA:**

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**31. MHESHIMIWA MBAROUK SALIM ALI (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Pamoja na Sheria kali ya udhibiti na usimamizi wa dawa za kulevya bado biashara hiyo ni tatizo kubwa kwa Tanzania:-

Je, ni nini mkakati mahususi wa Serikali wa kupambana na kadhia hiyo.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 32. MHESHIMIWA ZAYNAB MATITU VULLU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Zaidi ya asilimia 30 ya wakazi wa mijini hupata chakula chao cha asubuhi, mchana na jioni kwa mama lishe, lakini mama lishe hao hunyanyaswa sana na Askari wa Mgambo wa Majiji na Miji kote nchini:-

Je, kwa nini Serikali isiandae mazingira mazuri na masafi ya kufanyia kazi zao na wao wakatozwa ushuru mdogo kuliko hali hii ya kuendelea kuwanyanyasa.

### 33. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ili kuboresha elimu Serikali inashirikiana na Mashirika mbalimbali ikiwemo UNICEF ambao wanatoa misaada kwa sekta ya elimu:-

(a) Je, kwa mwaka 2014/15 msaada wa UNICEF kwa Halmashauri ya Mbeya ulilenga mahitaji gani ya kuboresha elimu;

(b) Je, ni kiasi gani na asilimia ngapi ya msaada huo ulitumika katika miradi ya maendeleo ya elimu;

(c) Je, ni kiasi gani na asilimia ngapi ya msaada huo ulitumika katika matumizi ya kawaida.

## WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

### 34. MHESHIMIWA MUNDE TAMBWE ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mpango mkakati gani kupitia Diplomasia ya Uchumi na nchi ya China kuunganisha wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ili kuingia ubia wa kuimarisha viwanda vidogo na vya kati.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 35. MHESHIMIWA SOPHIA MATHAYO SIMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Hali ya Magereza nchini ni mbaya hivyo kufanya vigumu katika utoaji wa haki za kibinadamu licha ya kwamba nchi imekuwa ikijali sana utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Kikanda na ya Kimataifa katika utoaji wa haki hizo kwa Wafungwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali hiyo katika Magereza nchini;

(b) Je, Serikali imejenga Magereza mapya mangapi katika kipindi cha miaka 20 iliyopita.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**36. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kampuni ya BG – EXXON MOBIL OPHIR na washiriki wenzao wako tayari kuanza ujenzi wa "LNG Plant":-

(a) Je, ni nini kinachokwamisha kuanza kwa utekelezaji wa mpango huo;

(b) Je, ni hatua gani za makusudi zinachukuliwa ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo.

**37. MHESHIMIWA OMARY AHMAD BADWEL (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye rasilimali mawe, mchanga na maji ambapo inapotokea Wakandarasi wanachukua rasilimali hizo au moja wapo kwa ajili ya ujenzi huchukua bure au kwa malipo kidogo na hivyo kuwakosesha haki Wananchi ya kunufaika na rasilimali hizo; hali hii ni

tofauti na maeneo yenye madini ambapo Wananchi hunufaika na uwepo wake:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka bei elekezi kwa Wakandarasi wanaohitaji mawe, mchanga au maji ili Wananchi wanaoishi maeneo yenye rasilimali hizo waweze kunufaika.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

**38. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-
Kituo cha Utafiti wa Malaria kilichopo katika Kata ya Vuje, Tarafa ya Gonja, Jimbo la Same Mashariki kilijengwa miaka ya 1960 na kina majengo ya kisasa kumi (10) na Serikali ilikifanyia ukarabati mkubwa Mwaka 2007 lakini mpaka sasa hakifanyi kazi badala yake kimegeuzwa kuwa nyumba za kulala wageni na pesa zinaingia mifukoni mwa watu wachache:-

Je, Serikali inalifahamu jambo hili na kama inalifahamu inatoa kauli gani.

**39. MHESHIMIWA AISHAROSE NDOGHOLI MATEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, iliagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kuanzisha maduka ya dawa kwenye Hospitali kubwa nchini:-

(a) Je, ni lini Serikali itaagiza MSD kufungua duka la dawa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ili kuwasaidia Wananchi kununua dawa kwa bei nafuu tofauti na zile zinazouzwa kwenye maduka ya mitaani;

(b) Je, ni lini Serikali itasambaza vifaa tiba vya kutosha kama vitanda vya wajawazito katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na Hospitali za Wilaya za Mkoa wa Singida.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**40. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Kakozi – Kapele mpaka Ilonga ina km 50.6 pia inaunganisha Mkoa wa Songwe na Rukwa bado

ipo chini ya Halmashauri pamoja na maombi ya kuipandisha hadhi kupitia vikao vyote ikiwemo Road Board kukubali:-

Je, ni kwa nini Serikali inachelewa sana kuipandisha hadhi barabara hiyo ili ihudumiwe na TANROADS kutokana na umuhimu wake.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa Mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016*).

**DODOMA** <br>
**08 SEPTEMBA, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH** <br>
**KATIBU WA BUNGE**